BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Pili – Tarehe 7 Februari, 2019.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

24. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hivi karibuni Serikali ilichukua hatua ya kupita katika shehia na mikoa ya Zanzibar ili kutoa elimu kwa wananchi na viongozi ili kujiepusha na migogoro ya ardhi inayojitokeza. Na kwa kuwa Serikali iliweka utaratibu wa mgawanyo wa mapato kwa fomu za uhaulishaji ardhi ambapo masheha wapewe shilingi 20,000/- kwa kila fomu.

Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea baadhi ya Mikoa fedha hizo kuingizwa Benki na baadae kutolipwa ipasavyo kwa masheha hao.

97. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kikosi cha Kuzuwia magendo KMKM wamekuwa wakifanya kazi zao vizuri za kupambana na watu wanaojihusisha na vitendo vya magendo na kuokoa pato la nchi yetu. Kwa kuwa Kikosi hicho kinafanyakazi nzuri ya kuzuwia mali mbali mbali za magendo nchini.

Je, kuna mpango wowote wa kuwapatia motisha pindi wanapokamata mali za magendo

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

42. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Kwa kuwa wananchi wetu hasa vijijini wamekuwa wakikosa baadhi ya haki zao kutokana na kutokujua sheria, jambo ambalo ni tatizo linaloweza kupelekea mtu kukosa haki yake Mahkamani.

(a) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuanzisha vituo vya sheria katika wilaya ili ipate kuwaelimisha wanajamii kuhusu haki zao.

(b) Je, kuna wanasheria wangapi kwa wilaya ya Micheweni ambao wamepangiwa kujitolea kutoa elimu ya sheria kwenye majimbo sambamba na kupeleka elimu ya sheria mashuleni ili watoto wetu wapatiwe uelewa wa sheria.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

5. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Pamoja na jitihada za Serikali kupitia agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutoa pencheni maalum kwa wazee wanaofikia umri wa miaka 70, ni jambo la kihistoria na kuwa mfano kwa nchi nyingi. Hata hivyo bado yapo malalamiko madogo madogo kwa baadhi ya watu kutokupata sadaka hiyo na umri wao uko tayari kupata haki hiyo.

(a) Je, Wizara imeshafanya utafiti kuona tokea kuanzishwa mfuko huo unatumika kama ulivyokusudiwa.

(b) Je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha fedha hizo haziendi kwa wajanja kwa wale wazee waliotangulia mbele ya haki.

Wizara ya Fedha na Mipango:

88. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Katika kuleta maendeleo Zanzibar hasa katika sekta za Ujenzi wa Majengo ya Serikali, Serikali hutoa Tenda kwa Makampuni ili kujenga majengo hayo. Hata hivyo, Serikali ina wataalamu inaowaamini wenye vyeti na sifa lakini bado hutoa fedha nyingi kwa Makampuni na baadhi yao hujenga majengo hayana viwango.

(a) Je, ni kwanini serikali inatoa tenda kwa Makampuni ya binafsi na wakati wataalamu wanao.

(b) Je, serikali haioni kutoa tenda kwa Makampuni ni kuongeza gharama na wataalamu wao wanao.

(c) Je, Serikali haioni kuajiri wataalamu na kutokuwapa kazi ni kuwadumaza utaalamu wao

Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

44. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa Kampuni za Utalii za nje na ndani ya Zanzibar zinafanya biashara mbali mbali za kiutalii ambazo zinasaidia kuutangaza utalii wetu. Na kwa kuwa zipo kampuni za nje ambazo hupokea wageni moja kwa moja nje na malipo yao na taratibu zote hufanyika nje ya nchi kabla ya mgeni kuingia Zanzibar.

(a) Je, kuna tozo gani zinazotolewa kwa kampuni za nje ambazo huleta wageni ndani ya nchi yetu wakiwa tayari wameshafanyiwa taratibu zote za huduma toka nchini kwao.

(b) Je, ni kiasi gani cha tozo wanayolipa Wakurugenzi wa kampuni za ndani na nje pale wanapotaka kutembelea sehemu za hifadhi zetu za Kitaifa

(c) Je, kuna tozo za aina gani wanazopaswa kulipwa na kampuni ya kupokea na kutembeza wageni ya ndani ya Zanzibar pale wanapotaka kutembelea maeneo ya kihistoria na yale ya Hifadhi ya Taifa.

144. MHESHIMIWA SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Inaeleweka kwamba katika moja ya ving'amuzi vinavyotumika hapa Tanzania vina chaneli ijulikanayo kama ZBC2 ambao ni chaneli inayoonesha masuala ya dini ya kiislamu na michezo.

(a) Je, chaneli hii ina uhusiano gani na Shirika la Utangazaji ZBC.

(b) Endapo zina uhusiano, kwa nini watangazaji wa chaneli hiyo ni tafauti na wale wa ZBC TV na ZBC Radio.

(c) Endapo hazina uhusiano, Shirika la Utanganzaji Zanzibar linapata manufaa gani kwa kutumiwa jina la ZBC ambalo ni maarufu ya Shirika la Habari la Zanzibar.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

6. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Pamoja na jitihada kubwa za Serikali kupiga marufuku ujenzi wa makaazi kwenye maeneo ya mabonde ya maji ili kuepuka maafa, baadhi ya watu hawatii amri ya Serikali na hivyo kusababisha maafa wakati wa mvua.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa wale waliojenga kwenye mabonde ambapo kumepigwa marufuku.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzuwia ujenzi wa nyumba za kuishi katika maeneo ya mabonde yanayojaa maji ili kuepusha matatizo yasitokezee.

(c) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu watu wanaojenga katika maeneo ya mabonde.

Wizara ya Afya:

141. MHESHIMIWA PANYA ALI ABDALLA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Hospitali ya Mnazi Mmoja ndiyo kimbilio letu wananchi wa Zanzibar kama Hospitali ya Rufaa ambapo matatizo makubwa yote yanatibiwa katika hospitali hiyo. Kumbukumbu za matibabu hubakia hapo ili wananchi akipata tatizo afuatilie jalada “file” lake na kuendelea na

matibabu. Kuna taarifa kuwa majalada “file” ya wagonjwa yanatiwa moto na wagonjwa kukosa taarifa zao.

(a) Je, jambo hili ni kweli.

(b) Kama ni kweli ni kwanini unapewa kipande chenye namba ya jalada, kipande kicho kina maana gani.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

29. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kutoka mkonga (*fiber optic*) kwa huduma ambazo zinatumiwa na kampuni binafsi.

(b) Je, katika kutumia huduma mbali mbali kwa kampuni binafsi, ni kiasi gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inadai na ni kampuni ngapi.

III. HOJA ZA SERIKALI

Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
7 Februari, 2019.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.